# ZABURI KWETU

ZABURI NA MASHANGILIO YA INJILI

TONI IRAGI K

## KWAREZMA

## MWAKA-C

MARS 2025


CANTEMUS PACEM DEI II

# ZABURI 50

## Siku ya tatu ya Majivu

Comp. : Ghislain Mapendano
Harm. & Psalm. :Toni Iragi K

PUERI CANTORES KAVUMU




1.Unihurumie, ee Mungu, kwa we**ma wako ;**
Kwa huruma yako kubwa, ufute mao**vu yangu.**
Unioshe kabisa ko**sa langu,**
Unisafishe pia za**mbi yangu.**

2.Kwa maana najua mao**vu yangu,**
Na zambi yangu ipo daima mbe**le yangu.**
Nimekukosea Wewe pe**ke yako,**
Nikatenda yaliyo mbaya mbe**le yako.**

3.Uniumbie moyo safi, **ee Mungu,**
utengeneze tena ndani yangu roho **imara.**
Usinitupe mbali na u**so wako,**
wala usiniondoshee roho yako ta**katifu.**

4.Unirudishie furaha ya woko**vu wako,**
unisabitishie roho **karimu.**
Unirudishie furaha ya woko**vu wako,**
unisabitishie roho **karimu.**

# Neno lako ee Bwana

## Siku ya Mungu ya Kwanza ya Kwarezma C

Musique : Toni Iragi K
Composé et publié en février 2024
Revu le 06 mars 2025
*Version corrigée*



# Zb 90 - Kaa pamoja nasi, ee Bwana

## Siku ya Mungu ya kwanza Kwarezma C

Toni Iragi K
Choeur Saint Grégoire le Grand
Paroisse de Karhale



# Zb 26 - Bwana ni mwanga wangu

## Siku ya Mungu ya pili Kwarezma C

Toni Iragi K




1. Bwana ni mwanga wangu na wokovu **wangu:**
nimwogope **nani?**
Bwana ni ukingo wa uzima **wangu:**
nimtetemekee **nani?**

2. Usikie, ee Bwana, sauti yangu ninayokuli**lia,**
unihurumie, unisiki**lize.**
Moyo wangu unakusemea **Wewe,**
uso wangu unakuta**futa.**

3. Ninautafuta uso wako, ee **Bwana:**
usinifiche uso **wako.**
Usimkatae kwa hasira mtumishi **wako:**
Wewe ndiwe msaada **wangu.**

4. Naaminia kuona wema wa **Bwana**
katika nchi ya wa**zima.**
Umtumainie Bwana, uwe hodari, uepe **moyo,**
unitumainie **Bwana.**

# Sifa kwa Kristu

## Acclamation de l'Evangile - 2è & 3è Dim. Carême C


Toni Iragi K



# Zb 102 Bwana ni mwenye huruma

## Siku ya Mungu ya tatu Kwarezma - C


Toni Iragi K



# Zb 33 - Onjeni mwone

Siku ya Mungu ya nne Kwaresma C

Toni Iragi K




1. Nitamtukuza Bwana kila **wakati,**
sifa yake kinywani mwangu **sikuzote.**
Roho yangu ijisifu ka**tika Bwana:**
wanyonge wasikie na **kufurahi.**


2. Mtukuzeni Bwana pamo**ja nami;**
tulikuze jina lake wo**te pamoja.**
Nilimkimbilia Bwana, akani**sikiliza,**
akaniopoa katika hofu **zangu zote.**

3. Mtazameni Yeye mfu**rahiwe,**
wala nyuso zenu zisi**huzunike.**
Mnyonge huyu alilia, naye Bwana a**kasikia,**
akamwokoa katika shida **zake zote.**

# Sifa na utukufu

## Acclamation de l'Evangile / 4è, 5è Dim. Carême - C
## & Rameaux / Matawi

Toni Iragi K



9

# Zaburi 125

**Siku ya Mungu ya tano ya Kwarezma C**

Toni Iragi K




1. Bwana alipowarudisha wafungwa wa Sio**ni,**
tulikuwa kama waota ndo**to.**
Hapo kinywa chetu kimejaa, kiche**ko,**
na ulimi wetu shangili**o.**

2. Hapo walisema kati ya matai**fa:**
Bwana amewatendea maku**bwa.**
Bwana ametutendea maku**bwa,**
tumeona fura**ha**.


3. Uwarudishe, ee Bwana, wafungwa we**tu,**
kama mito jangwani mwa kusi**ni.**
Wanaopanda mbegu wakilia macho**zi,**
watavuna kwa sha**ngwe.**


4. Kwenda wanakwenda kwa kulia macho**zi,**
wakichukua mbegu za kupa**nda;**
kurudi wanarudi kwa sha**ngwe**
wakichukua miganda ya**o.**


# Zb 21 - Mungu wangu, kwanini umeniacha ?

Siku kuu ya Matawi, ya Mateso ya Bwana

Toni Iragi K



# Zb 115-Vibarikiwe

## Siku ya Nne Takatifu

Toni Iragi K




1. Nimrudishie Bwana ni**ni**
kwa yote aliyonitende**a ?**
Nitainua kikombe cha woko**vu,**
nitaliomba jina la Bwa**na.**

2. Kina bei kubwa machoni pa Bwa**na**
kifo cha waamini wa**ke.**
Ee Bwana, mimi mtumishi wa**ko,**
umenifungulia vifu**ngo.**

3. Nitakutolea sadaka ya si**fa,**
nitaliomba jina la Bwa**na.**
Nitamtimizia Bwana naziri za**ngu**
mbele ya taifa lake lo**te.**

# Sifa na utukufu

## Siku ya nne na siku tano takatifu
## Acclamation Jeudi & Vendredi Saint

Toni Iragi K



# ZB 30-Naweka roho yangu

Siku ya tano takatifu
Vendredi Saint

Toni Iragi K




1. Nakukimbilia Wewe, ee Bwa**na:**
Nisione haya mile**le**
Naweka roho yangu mikononi mwa**ko,**
Utaniokoa, ee Bwana, Mungu mwamini**fu.**

2. Nimechekwa na adui zangu wo**te,**
na kufanyiziwa mzaha na majirani wa**ngu ;**
ninakuwa kitisho kwa rafiki za**ngu,**
wenye kuniona njiani wananikimbi**a**.

3. Nimesahauliwa na watu kama **mfu,**
kama chombo kilichotu**pwa**
nimesikia masingizio ya wa**tu**
Wameshauriana kuniondoa uzi**ma.**

4. Mimi lakini nakuaminia, ee Bwa**na.**
Nasema: “Ndiwe Mungu wa**ngu”**
Maisha yangu yamo mkononi mwa**ko,**
uniponye na mikono ya adui zangu na wazulumu wa**ngu.**


5. Umwangazie mtumishi wako uso wa**ko,**
unisalimishe kwa wema wa**ko!**
Muwe hodari, shikeni mo**yo,**
enyi wote mnaomtumainia Bwa**na!**

# Zaburi 32

## Kiisha somo la kwanza la makesha ya Pasaka

Parokya ya Karhale/Bukavu
Shirika la heri kwetu
Bienheureuse Anuarite

**Musiki wa Toni Iragi K**




1. Neno la Bwana ni la **kweli,**
matendo yake yote ni maamini**fu,**
Anapenda unyofu na **haki;**
dunia imejaa wema wa**ke Bwana.**

2. Mbingu zimefanywa kwa neno la **Bwana,**
na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa cha**ke**,
Anakusanya maji ya baharini kama kiri**bani,**
anaweka vilindi mabi**rikani.**

3. Heri taifa lenye Bwana ni Mungu **wake,**
kabila alilochagua kuwa urisi wa**ke.**
Toka mbinguni bwana anata**zama,**
anaona waana wote **wa watu.**

4. Roho yetu inamngojea **Bwana,**
Yeye ndiye msaada wetu na ngao ye**tu.**
Huruma yako, ee Bwana, itushu**kie,**
kama vile tunavyokutuma**inia.**

# Zb 103-Tuma roho wako ee Bwana

Kiisha somo la kwanza
Makesha ya Pasaka

Toni Iragi K




1. Umsifu Bwana ee ro**ho yangu:**
ndiwe mkubwa sana, ee Bwana, Mungu wa**ngu.**
Umevaa ungaro na u**tukufu,**
umejivika mwanga ka**ma vazi.**

2. Umeweka dunia juu ya mawe**ko yake:**
haitatikisika na milele na mile**le.**
Uliifunika kwa kilindi ka**ma vazi,**
maji yalisimama juu ya **milima.**

3. Umetokeza chemchemi zichururike ma**bondeni,**
zitiririke kati ya mili**ma.**
Kandokando wanakaa ndege za **angani,**
wanatoa sauti kati ya **matawi.**


4. Unanywesha milima toka maka**o yako**
dunia inashiba mazao ya matendo ya**ko;**
unaotesha majani kwa ajili ya **wanyama,**
na mimea kwa matumizi ya wa**nadamu**


5. Kazi zako ni nyingi sana, **ee Bwana:**
zote umezifanya kwa heki**ma.**
Dunia imejaa viu**mbe vyako:**
umsifu Bwana, ee ro**ho yangu.**

# Zb 15-Ee Mungu unilinde

Kiisha somo la pili
Makesha ya Pasaka

Toni Iragi K




1. Bwana ndiwe urisi wangu na kikombe cha**ngu,**
   ndiwe unayenilinda ukomo wangu mkononi mwa**ko.**
   Namweka Bwana daima mbele ya macho ya**ngu**
   Sitatikisika, kwa maana yupo kuumeni kwa**ngu**

2. Kwa hiyo moyo wangu waona furaha, nayo roho yangu yatoa sha**ngwe,**
   hata mwili wangu utapumzika sala**ma,**
   kwani hutaiacha roho yangu kuzimu**ni**
   Wala hutamkubali mwamini wako aingie shimo**ni.**

3. Ee Mungu, nakukimbili**a**
   Unanionyesha njia ya uzi**ma,**
   wingi wa furaha mbele ya uso wa**ko,**
   anasa za milele kuumeni kwa**ko.**

# Kutoka 15-Namwimbia Bwana

## Kiisha somo la tatu Makesha ya Paska

Toni Iragi K




*1.Bwana ndiye nguvu yangu na wimbo wangu,amenipa woko**vu.***
*Ndiye Mungu wangu, nina msi**fu,***
*Mungu wa baba yangu, ninamtuku**za.***
*Bwana ni hodari wa vita: jina lake ni Bwa**na.***

*2.Magari ya Farao na jeshi lake amewatupa bahari**ni;***
*maakida wake wateu**le***
*Bahari Nyekundu iliwame**za.***
*Vilindi vimewafunikiza, walizama chini kama ji**we.***


*3.Mkono wako wa kuume, ee Bwa**na,***
*umejitukuza kwa nguvu: wa kuume wako, ee Bwana,/*
*umewavunja maadu**i.***
*Ulipuliza pumzi yako, bahari ikawafuniki**za:***
*wakazama kama risasi katika maji maku**u.***


*4.Utawaingiza watu wako na kuwapandikiza mlimani pa urisi wa**ko:***
*mahali ulipofanya pawe makao yako,mahali patakatifu, ee Bwa**na,***
*palipotengenezwa na mikono ya**ko.***
*Bwana atatawala milele na mile**le.***

# Zb-29-Nakutukuza ee Bwana

Kisha somo la Nne-Makesha ya Pasaka

Toni Iragi K




1. Nakutukuza, ee Bwana, kwa kuwa umenio**koa,**
wala hukuwafurahisha adui zangu juu **yangu.**
Ee Bwana, umeondoa roho yangu kuzi**muni,**
umeniokoa katika wale wanaoshuka **shimoni,**


2. Mwimbieni Bwana, enyi waamini **wake,**
shukuruni jina lake litaka**tifu.**
Kwani hasira yake ni ya kitambo ki**dogo,**
mapendo yake yadumu mai**sha yote.**

3. Usikie, ee Bwana, unihuru**mie,**
ee Bwana, uwe msaada **wangu.**
Umegeuza kilio changu kuwa **mchezo,**
ee Bwana, Mungu wangu, nitakusifu **milele.**

# 5.Yesaya-12-Mtachota maji

## Kiisha somo la tano-Makesha ya pasaka


Toni Iragi K



1. Sasa Mungu ni Mwokozi wangu,
namtumainia, wala sina hofu tena.
Kwa kuwa Bwana ni nguvu yangu na wimbo wangu,
Bwana amekuwa wokovu wa**ngu.**

2. Nanyi mtachota maji kwa furaha/visimani mwa wokovu.
Mtukuzeni Bwana, liombeni jina lake,
tangazeni matendo yake kati ya mataifa,
wakumbusheni ya kuwa jina lake ni tuku**fu**.

3. Mwimbieni Bwana, maana ametenda makuu,
nayo yatangazwe duniani kote.
Pigeni kelele za furaha na shangwe, wenyeji wa Siyoni,
maana ametukuzwa ndani yenu Mtakatifu wa Israe**li.**




# Zaburi 18 - Ee Bwana unayo maneno.


## Kiisha somo la sita la makesha ya Pasaka

**Parokya ya Karhale/Bukavu**
**Shirika la heri kwetu**
**Bienheureuse Anuarite**

Musiki wa Toni Iragi K




1.Sheria ya Bwana ni kami**lifu,**
yatuliza **roho**
mafundisho ya Bwana ni i**mara**,
yamletea mjinga e**limu.**

2. Amri za Bwana ni za **haki,**
zafurahisha **moyo;**
agizo la Bwana ni **safi,**
layatia macho mwa**ngaza.**

3. Ibada kwa Bwana ni **safi,**
yadumu hata mi**lele;**
hukumu za Bwana ni **kweli,**
zote za haki ka**mili.**

4. Zatamanika kuliko za**habu,**
kuliko wingi wa zahabu **safi;**
ni tamu kuliko a**sali,**
kuliko mavuno ya **uki.**

# Zb 41-Roho yangu inaona kiu

## Kiisha somo la saba-Makesha ya Pasaka

**UBATIZO USIPO FANYWA**
**S'il n'y a pas Baptême**

Toni Iragi K




1. Kama swala anavyotamani mito **ya maji,**
ndivyo roho yangu inavyoku**tamani**
ndivyo roho yangu inavyoku**tamani**
Wewe, **ee Mungu.**

2. Nakumbuka hiyo, jinsi nilivyokwenda he**kaluni,**
na kuandamana nyumbani **kwa Mungu,**
kati ya kelele za shangwe **na sifa,**
kati ya sherehe ya ma**kutano**

3. Ulete mwanga wako na uamini**fu wako,**
nao uni**ongoze,**
unipeleke kwenye mlima wako mta**katifu**
palipo maka**o yako.**


4. Nitakwenda altareni **kwa Mungu,**
kwa Mungu wa fura**ha yangu.**
Nitakusifu kwa kukupigia **kinubi,**
ee Bwana, Mu**ngu wangu.**

# Zb 50-Uniumbie moyo safi

Kiisha somo la saba - Makesha ya Pasaka

**IKIWA KUNA UBATIZO**
**S'il y a baptême**

Toni Iragi K




1. Uniumbie moyo safi, ee Mu**ngu,**
utengeneze tena ndani yangu roho ima**ra.**
Usinitupe mbali na uso wa**ko,**
wala usiniondoshee roho yako takati**fu.**

2. Unirudishie furaha ya wokovu wa**ko,**
unisabitishie roho kari**mu.**
Nitawafundisha waasi njia za**ko,**
nao wakosefu watakuongoke**a.**

3. Kwa maana hupendezwi na sada**ka;**
ningetoa sadaka ya kuteketezwa, hungeipoke**a.**
Sadaka yangu, ee Mungu, ni roho ya kutu**bu:**
moyo wenye kutubu na kupondeka, ee Mungu, hutauzara**u**.

# Zb-117 Aleluya Bwana ni mwema

Kiisha somo ya Waraka

Toni Iragi K




1. Mshukuruni Bwana kwani ndiye mwe**ma,**
Kwani wema wake ndio wa mile**le**. ALELUYA

Wenye kumwabudu Bwana wase**me:**
Kweli wema wake ndio wa mile**le.**ALELUYA

2. Mkono wa kuume wa Bwana umetuku**zwa**
Mkono wa kuume wa Bwana umetenda maku**bwa**.ALELUYA

Sitakufa, lakini nitai**shi,**
tena nitahubiri matendo ya Bwa**na**.ALELUYA

3. Jiwe walilokataa wajenga**ji,**
hilo limekuwa jiwe la pe**mbe :** ALELUYA

Ndilo jambo alilofanya Bwa**na,**
nasi twaliona aja**bu.** ALELUYA